Tangu Wakati Huo

Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utabariki kukusanyika kwetu usiku wa leo. Na iwe kwamba kama, kwa bahati, kuna wale hapa ndani ambao hawajamjua Yeye kama Mwokozi wao, jalia jambo fulani lifanyike, usiku wa leo, litakalomleta Yeye halisi sana kwao hata atakuwa kwao asiyeweza kukataliwa. Jalia waone Yeye ni mtamu na wa thamani nafsini mwao, kama vile sisi, watumishi Wako, tulivyomwona.

2 Tungeowaombea hasa, Bwana, wale walio hapa ambao ni wagonjwa na wahitaji. Baadhi yao, hapana shaka, wako karibu na kufa. Matabibu wa thamani wa dunia hii wamefanya yote wajuayo kufanya, hakuna msaada, basi tunakuja Kwako, Ee Yehova-Yire na Yehova-Rafa, tunaomba ya kwamba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utatimiza mambo haya tunayoomba, usiku wa leo.

3 Tungewakumbuka wale wanaopata nafuu na hawawezi kutoka, jalia Roho Mtakatifu awazuru hospitalini, na nyumbani kitandani, wakiteseka. Jalia rehema Yako itutawale, Baba. Nasi tutakupa sifa, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, Bwana Yesu. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

4 Ketini. Ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo, na kuhudumu tena katika Jina la Bwana wetu wa thamani.

5 Nilikuwa na majaliwa, dakika chache zilizopita, kuzungumza na mke wangu na mtoto wangu Joseph, yule mvulana mdogo ambaye ninaamini ya kwamba Mungu atamruhusu kuchukua mahali pangu nitakapomaliza maisha haya.

6 Kwa hiyo tuna bahati sana leo, kuishi katika siku hii, kuona kukaribia kwa Kuja kwa Bwana.

7 Jana jioni ilikuwa jioni isiyo ya kawaida sana. Kila jioni na kila dakika pamoja na Bwana Yesu si ya kawaida. Nasi tunaninii, tunaweza kutarajia karibu kitu chochote kutukia wakati Uwepo Wake wa neema ukiwa karibu.

8 Sasa, yale mambo madogo tunayofanya, kumwalika mtu kwenye mkutano:

> Sema neno dogo kwa ajili ya Yesu,
> Shuhudia, imba, au uombe,
> Na kama mkate juu ya maji,
> Itakurudia siku moja.

9 Wakati mwingine tunajisikia kwamba kama sisi, si mtu fulani mkubwa ambaye hatuwezi kufanya vya kutosha, lakini ninaamini imeandikwa katika Maandiko ya kwamba si mambo

makubwa tunayofanya, ni mambo madogo tunayoacha bila kufanya. Lakini Yesu anajua kila kitu kidogo unachofanya.

10 Wakati fulani uliopita huko Canada, huko Vancouver, naamini ilikuwa, marehemu Mfalme George alikuwa akifanya ziara yake huko Canada. Alasiri hiyo, kuonyesha uaminifu kwa mfalme wao, wa—watoto wa Canada wote walikuwa wameachiliwa kutoka kwenye shuleni zao, nao wakachukua bendera zao ndogondogo, bendera zao ndogondogo za Uingereza, na kusimama mtaani kumpeperushia mfalme mkuu, mwenye nguvu alipokuwa akipita.

11 Onyesho hilo daima lilikuwa na mambo mawili kwangu. Malkia wake mpendwa, bila shaka, alikuwa ameketi karibu naye amevaa vazi lake zuri, la bluu. Naye alikuwa akiugua wakati huo, hiyo ilikuwa kabla hajaponywa, ugonjwa wa tumbo, naye alikuwa na ugonjwa wa sirosisi, pia, naye alikuwa ameketi, na ungeweza kujua usoni mwake kulikuwa na maumivu. Bw. Baxter, mwenzangu, alikuwa akisema wakati alipokuwa amepita, walipopita, aliweka tu mikono yake usoni mwake akaanza kulia.

Bila shaka, mimi, mwenyewe, sikujua sababu yoyote ya kulia, bali alisema, "Wazia hilo, mfalme wetu anapita."

12 Basi nikawazia, kama hilo lingemfanya Mkanada alie kumwona mfalme wao, Mfalme George, akipita, itakuwaje wakati Mfalme wetu Yesu atakapokuja? Litatupa ushawishi wa—wa namna gani?

13 Watoto wadogo wakipeperusha bendera zao, na baada ya huyo mfalme kupita, mbona, wote walikuwa warudi shuleni. Basi wote wakarudi, ila katika shule fulani, msichana mmoja mdogo hakuwepo. Kwa hiyo mwalimu, akihofu, alikimbia mtaani, akiliita jina lake, akijaribu kutafuta mahali alipokuwa, na baada ya kitambo kidogo akamkuta ameinamisha maskini kichwa chake kwenye nguzo ya simu, akilia sana.

14 Ndipo mwalimu akamkimbilia, na kumshika mikononi mwake, na kusema, "Kuna nini, mpenzi? Kwani hukumwona mfalme?"

Naye akasema, "Naam, nilimwona mfalme."

Kasema, "Vema, hivi hukuweza kumpeperushia bendera yako?"

Kasema, "Nilipeperusha bendera yangu."

Kasema, "Vema, kwa nini unalia?"

15 Akasema, "Unaona, mwalimu, mimi ni mdogo, nami nikiwa mdogo sana nilipeperusha bendera yangu, na nikapiga mayowe, lakini," kasema, "nilimwona mfalme, bali mfalme hakuniona." Alikuwa mdogo sana.

16 Lakini huwezi kufanya jambo lolote dogo sana, pasipo Yesu kuliona, haidhuru liko wapi, ni nini, ushuhuda wowote mdogo au onyesho la uaminifu kwa Yesu. Anajua shomoro anayeanguka barabarani, anajua mawazo yenyewe ya moyo. Biblia ilisema ya kwamba—ya kwamba Yeye aliwajua shomoro walioanguka barabarani. Nasi tuna furaha sana kujua jambo hilo, ya kwamba kila jambo dogo tunalofanya, Yesu anatuona tukilifanya. Naye anajua kusudi na nia tuliyo nayo ndani yake, Naye atatupa thawabu.

17 Wakati mmoja Yeye alisema, "Amin, nawaambia, mkimnywesha mmojawapo wa hawa angalau kikombe cha maji baridi, haitawapotea kamwe thawabu yenu," mambo madogomadogo ambayo tunasahau tu. Usisahau, unapomwona mlemavu mtaani, maskini, kipofu, na kiwete, au mlemavu, badala ya kumtumbuiza mtu fulani, msaidie. Yesu alisema, "Nalikuwa mgonjwa, msije kunitazama; nilikuwa kifungoni, msije kunitazama; nilikuwa na njaa, msinipe chakula."

"Tulikuwa namna hii lini? Tulikuona lini?"

18 "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hawa, mmenitendea Mimi." Loo, jinsi tunavyopaswa kumshukuru Bwana wetu Yesu wa thamani!

19 Sasa, usiku wa leo, Ndugu David ndiye anayehubiri, nami nina kitu kidogo—kidogo tu mwishoni. Hatujagawa kadi zozote za maombi, bado. Kuna wagonjwa wowote hapa? Inueni mikono yenu kama kuna wagonjwa. Tulizigawa hivi majuzi usiku, kisha tukazikusanya zote. Na sasa je, mngetaka kuwa na mstari wa maombi, halafu kesho usiku? Kama mngetaka, inueni mikono yenu, ninyi. . .Ninataka kuona vile ninyi nyote mnavyowazia. Kama mngetaka mstari wa maombi, kupewa kadi za maombi, nitawatuma wale wavulana washuke wakazigawe. Kama unaitaka, inueni tu mikono yenu. Vema. Vema, tutawaacha wasambaze kadi za maombi basi, kesho usiku, tena. Yapata saa kumi na mbili u nusu ndio mnazigawa? Saa kumi na mbili na nusu. Vema. Hiyo itakuwa sawa.

20 Laiti mngefungua Maandiko, kama una Biblia yako karibu, na kufungua mlango wa 4 wa Mathayo Mtakatifu. Hebu na tusome pamoja kwa muda kidogo, kifungu cha 16 na cha 17:

> Na *watu wale waliokaa katika giza wameona mwanga mkuu; na* hao *walioketi katika nchi na uvuli wa mauti, mwanga. . .umewazukia.*
>
> *Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni: kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*

21 Ninataka kuchukua maneno matatu ya kwanza ya mlango wa 17: *Tangu Wakati Huo*, maneno hayo matatu, *Tangu Wakati Huo*, kwa wazo dogo kwa dakika chache tu.

22 Mwajua, kama mvulana mdogo, ama msichana, mtoto, mambo fulani hutukia ambayo tunaweza kuelekeza nyuma, na kusema, "Tangu wakati huo, tulifanya *hili-na-hili*. Jambo *hili-na-hili* lilitukia na tangu wakati huo ikawa *hivi-na-hivi*."

23 Na labda, mwanamke mtovu wa uadilifu, angeweza kusema kitu kama hiki: "Nilikuwa msichana mwadilifu, nililelewa katika nyumba ya Kikristo yenye nidhamu, na baba na mama watauwa, nami nilikuwa safi tu kama yungiyungi, mpaka usiku mmoja niliposafiri pamoja na mvulana fulani. Nasi tukaendesha gari hadi kwenye ukumbi wa dansi, na tangu wakati huo." Sikuzote unarejelea wakati fulani ambapo jambo fulani lilitukia.

24 Hapa, si muda mrefu uliopita, nilikuwa katika Jiji la New York pamoja na Dk. Berg, alikuwa mchungaji wa Maskani ya Bethel. Nao wana misheni huko chini Bowery, nami sikuzote nilitaka kutembelea Bowery. Nilishuka kwenda barabarani pamoja naye, na, loo, ilikuwa kama nilivyozoea kusikia kama mvulana mdogo, wimbo:

> Ni picha ya upande wa pili wa maisha,
> Mtu ambaye ameanguka njiani,
> Mtu aliyechukuliwa na mkondo wa maji
> Ambaye huenda ikawa siku moja alikuwa na
> furaha.

25 Kulikuwako na watu waliokuwa wamelala chini ya benchi hilo kubwa, baadhi yao wakiwa hoi kabisa, wamelala mtaani katika, loo, hali mbaya sana, najisi, Chinatown, chini yake tu, ambako wangenunua dawa zao za kulevya. Ndipo nikamwambia Dk. Berg, nikasema, "Labda watu hawa wanatoka kwenye nyumba mbaya sana wala kamwe hawakupata nafasi."

26 Akasema, "Inashangaza sana, Ndugu Branham, watu hao, wengi wao ni watu mashuhuri." Kisha akasema, "Hapa, jamaa huyo aliyelala pale," kasema, "ninamjua," kasema, "hebu tuone kama tunaweza kumwamsha."

27 Basi nikaenda pale na kumtikisa. Nayo masharubu yake, yamejaa mvi usoni mwake, huku—huku vitu vikitiririka kutoka kinywani mwake, na shati lake likiwa chafu, naye karibu ananuka kama zizi la nguruwe. Nikawazia, "Huenda akawa ni baba wa mtu fulani, maskini mtu fulani aliyeanguka njiani."

Basi nikasema, "Jina lako ni nani?" Naye alitaka nimpe pesa za pombe.

28 "Loo," nikasema, "nisingeweza kufanya hivyo, bwana, mimi ni mhudumu, wala kamwe ni—nisingeweza kukupa pesa za pombe. Nitakununulia chakula." Nikasema, "Hebu niambie, ilikuwaje? Kwani sikuzote ulikuwa katika hali hii?"

"La, bwana." Basi akaanza kuzungumza nami. Naye akasema, "Ati wewe ni mhudumu?"

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Nisaidie kuinuka.”

29 Ndipo nikamkumbatia kwa mkono wangu, na kujaribu kumsimamisha. Alikuwa hoi sana, kidogo—kidogo alichuchumaa tu mtaani kisha akaanguka, nikainama chini, nikamwegemeza begani mwangu.

30 Akasema, “Bwana, hutaki kuamini hadithi yangu, nadhani,” lakini kasema, “si zaidi ya majengo matano ya mji kutoka hapa, nilikuwa rais wa benki ile.”

Nikasema, “Bwana, hiyo ni kweli?”

Akasema, “Waulize.”

Nami nikasema, “Ilikuwaje?”

31 Akasema, “Nilikuja nyumbani siku moja, ambako nilikuwa na familia nzuri sana,” ila kasema, “Nilipata barua ya ‘Mpendwa Yohana’ mezani.” Akasema, “Nilimpenda sana nisingeweza kumsahau, na tangu wakati huo.”

32 Haya basi. “Tangu wakati huo,” kitu fulani kinautia alama.

33 Unaweza kumwuliza mlevi, mlevi sugu, “Ulianza kunywa pombe lini?”

34 “Loo, sikuwahi kunywa pombe maishani mwangu, mpaka usiku mmoja nilikuwa huko nje na kundi la wenzangu kwenye sherehe ndogo, nami nikanywa pombe yangu ya kwanza, na tangu wakati huo.” Hivyo ndivyo iendavyo, huanza wakati fulani.

35 Hapa wakati fulani uliopita, katika . . . tulikuwa na vita vya dunia, Vita vya Kwanza vya Dunia, baada ya vita hivyo kwisha, waliunda kile kilichoitwa Shirikisho la Mataifa. Mbona, nilikuwa tu mvulana mdogo, lakini ninakumbuka nikiwasikia wahudumu wakisema, “Hatutakuwa na vita tena, kwa sababu tumeweka wakati ambapo tutaulinda ulimwengu mzima kwa hili Shirikisho la Mataifa.” Lakini halikufanya kazi.

36 Wana UN sasa, lakini ha—haifanyi kazi hata sasa, haitafanya kazi. Watu hujaribu kufanya jambo fulani, ndipo . . .

37 Kama vile, nilizungumza na mama mmoja, hapa, si muda mrefu uliopita, akijaribu kuiunganisha nyumba yake pamoja tena. Nikasema, “Mlete mumeo mje mnione.”

Akasema, “Siwezi kufanya hivyo, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Kwa nini usiweze kufanya hivyo?”

Akasema, “Sitaki kukabiliana na hayo tena. Hivi utaenda ukazungumze naye, uone kama atanirudisha?”

Nikasema, “Kuna nini mbaya hivyo?”

38 Kasema, “Ndugu Branham, mimi na John tulioana, nilikuwa na maadili mema kama mwanamke angeweza kuwa.” Kisha kasema, “Tukahamia ujirani, na tukaenda kanisani, na kufanya

yaliyo mema. Lakini siku moja muuzaji mrefu, mweusi, mwenye sura nzuri alibisha mlangoni pangu, nami nikamkaribisha ndani, na tangu wakati huo. Kila mwaka mpya," anasema, "nimejaribu kujilainisha na kuanza tena."

39 Hapa, siku moja, niliingia kwenye chumba cha dharura katika jengo fulani, nalo lilidhaniwa kuwa ni la wendawazimu. Nilipoingia mlangoni, kulikuwako na msichana mzuri, mrembo, mwenye umri wa kama miaka ishirini na mitano ameketi pale akiniangalia. Nikasema, "U hali gani?" Na baadhi yao ni wenye kichaa, na ndevu zimefunika nyuso zao, huku wakilaani, na, loo, wamejawa na nguvu za pepo. Nami nikamwangalia, nikasema, "Vema, kidogo ni vigumu kujua mahali pa kuanzia kuombea kwanza."

Akasema, "Kama hujali, laiti ungeanza na mimi."

Nikasema, "Ati na *wewe*?"

Kasema, "Naam, bwana."

Nikasema, "Wewe si mgonjwa!"

Akasema, "Mimi ni mgonjwa, bwana."

Nikasema, "Vema, una shida gani?"

Akasema, "Nadhani nina kichaa."

Nikasema, "Kwa kweli huonekani hivyo."

Akasema, "Waweza kusikiliza hadithi yangu?"

Nikasema, "Bila shaka."

40 Naye akasema, "Nilipokuwa msichana mdogo, Ndugu Branham, nililelewa katika nyumba halisi ya Kikristo. Halafu nikaanza kuambatana na mvulana aliyevuta sigara." Kisha kasema, "Muda si muda unajua nilikuwa nikivuta sigara. Ndipo usiku mmoja alichanganya wiski kwenye Koka, na hapo nikaanza kunywa pombe." Akasema, "Tokea hapo nikaanza ukahaba." Naye akasema, "Nimeishi kwenye mifereji ya takataka za kuzimu yenye giza sana."

41 Akasema, "Nilitumikia miaka minne katika hospitali ya Katoliki, Nyumba ya Mchungaji Mwema." Kisha kasema, "Mle ndani, nikafungua ukurasa mpya, nami nikasema, 'Nitakapotoka hapa, nitatembea nikiwa imara.'" Kasema, "Nililimaanisha, lakini mara nilipoungana na umati tena, yote yalikuwa yamekwisha. Halafu," kasema, "nilitumikia miaka miwili katika gereza la serikali la wanawake, hapa katika jimbo hili."

42 Halafu akasema, "Hapo nikawazia, kweli nilikuwa nimebadilika. Nikaja nyumbani na kujiunga na kanisa lingine. Nikamwambia mchungaji, tukashuka kwenda madhabahuni na kulizungumzia, lakini," akasema, "Siwezi tu kuyaacha." Akasema, "Ilianzia usiku mmoja."

43 Nikasema, “Mama, hivi hutaki kuwa mama halisi mwenye heshima, na kuwa na mume na watoto wachanga, kama vile mwanamke halisi angetaka?”

Akasema, “Loo, kwa moyo wangu wote.” Akasema, “Lakini niangalie sasa.” Nikasema. . . Akasema, “Nimejaribu na kujaribu.”

Nikasema, “Lakini hujamjaribu Bwana wangu, bado.”

Akasema, “Naam, nimemjaribu, pia, Ndugu Branham.” Kasema, “Nimetia sahihi ahadi na nadhiri, nikamtolea Mungu ahadi nyingi.”

Nikasema, “Hilo silo ninalozungumzia.” Ndipo nikasema, “Kadiri inavyoonekana ya mtindo wa kale, ni ibilisi.”

Akasema, “Sikuzote nimeamini hilo.”

Nikasema, “Yeye anakusukuma kufanya mambo usiyotaka kufanya.”

Akasema, “Ninaamini hilo.” Kisha akasema, “Je, kuna tumaini kwangu?”

Nikasema, “Bila shaka,” kisha tukapiga magoti kuomba.

44 Baada ya kitambo kidogo, akasimama, mwanamke mrembo, macho makubwa laini, akaangalia juu, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, naye akasema, “Sasa, Ndugu Branham, ni—ninaamini nitatoka niende nikaishi maisha mapya.”

45 Nikasema, “Dada mpendwa, unafungua tu ukurasa, haitafaa chochote,” Nikasema, “umefanya hivyo mara nyingi sana.” Nikasema, “Kaa tu hapa mpaka Mungu atakapokujibu.”

46 Tukainama pale pamoja na kuomba. Nami nikamwacha akiomba, nikasonga mbele, kuomba pamoja na watu wengine. Baada ya kitambo kidogo akasimama kutoka pale na kuangalia pande zote chumbani, hayo macho makubwa yakiniangalia, akasema, “Jambo fulani lilinitendekea!”

47 Nikasema, “Sasa umelipata! Sasa umelipata! Haikubidi kufungua kurasa mpya sasa, imetendeka. Umelipata.” Na tangu wakati huo, alikuwa mtu aliyebadilika. Ameolewa, ana nyumba nzuri, na watoto wawili sasa. Anaweza kuelekeza vidole vyake kwenye wakati ambapo jambo fulani lilimpata ambalo lilikuwa ni la milele.

48 Mambo hutokea na maisha yanabadilika, lakini kuna jambo fulani linaloweza kumpata mtu, ambalo halitabadilika, huwezi kuwa vile vile baada ya jambo hili kutukia: hapo ni wakati mwanadamu anapokutana na Mungu. Anabadilishwa, jambo fulani linampata. Yeye hayuko vile vile baada ya kukutana na Mungu, uso kwa uso, ambapo hana budi kuufikia ukweli wa ama kumpokea, au kuondoka Kwake. Ataondoka, vema, akiwa mtu mbaya zaidi, ama aondoke akiwa mtu mpya. Lakini

unapokutana na Mungu, jambo fulani hutokea, lisilopatikana na mauti.

49 Hebu tuwaite tu wachache usiku wa leo, ambao tunajua wamekutana na Mungu. Hebu tumchukue baba Ibrahimu. Alikuwa tu ni mtu wa kawaida. Alishuka kutoka, labda baba yake, huko juu karibu na Babeli, naye alikuwa mzee, yapata umri wa miaka sabini na mitano, hakuna kitu kizuri sana kwake. Lakini Mungu, kwa uteuzi, aliona kitu fulani ndani yake, ndipo Mungu akamtokea, naye akawa mtu aliyebadilika.

50 Kuna jambo fulani kulihusu, Mungu anapomtokea mtu, yeye ni kiumbe kilichobadilika tangu wakati huo na kuendelea. Na wakati mwingine Yeye hukufanya ufanye mambo ambayo hukuwazia ungeyafanya, unapokutana na Mungu.

51 Ungeweza kuwazia mzee wa miaka sabini na mitano, Ibrahimu, na mkewe miaka sitini na mitano, walikuwa wameishi pamoja tangu, alikuwa ni dada yake wa kambo, walikuwa wakiishi pamoja tangu walipokuwa vijana na wachanga. Na sasa, hawa hapa, umri wa miaka sitini na mitano, amekoma hedhi kwa muda wa miaka kama ishirini, naye Ibrahimu, umri wa miaka sabini na mitano, ndipo Mungu akakutana na Ibrahimu na kumwambia atapata mtoto kwake, nao wakajiandaa kwa ajili ya mtoto huyu mchanga.

52 Ungeweza kuwazia mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano akishuka kwenda hospitalini, na kumwona daktari, na kufanya mipango ili yeye na mke wake wa miaka sitini na mitano wapate mtoto, akija hospitalini? Watu wangesema, huyo daktari angesema, "Huyo mzee kidogo amerukwa na akili." Lakini alikuwa amekutana na Mungu, hilo ndilo lililoleta tofauti.

53 Wakati mwingine unapokutana na Mungu, Yeye anakufanya uamini mambo ambayo akili ya kawaida haiwezi kuyawazia. Kuna kitu fulani kumhusu Yeye, unapokutana Naye, kinakubadilisha, kinakufanya mtu tofauti, unaangalia kwa macho tofauti tangu wakati huo na kuendelea.

54 Ungeweza kuwazia, bikizee mwenye umri wa miaka sitini na mitano, ameketi kitako, akishona vijiatu vidogo, akifanya maandalizi kwa ajili ya mtoto mchanga? Mbona, hao wanawake wangelisema, "Huyo bikizee amerukwa na akili," bali alimwamini Mungu, nao wakampata huyo mtoto miaka ishirini na mitano baadaye. Naye bado alikuwa anamngojea, badala ya kuwa mnyonge zaidi.

55 Sasa, tunajiita Uzao wa Ibrahimu. Naye Ibrahimu alimwamini Mungu alipokutana Naye na kuzungumza naye. Na kama tuko ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu na warithi pamoja naye, sawasawa na ile ahadi. "Kwa imani Ibrahimu alimwamini Mungu, na kuyaita yasiyokuwako, kana kwamba yalikuwako," kwa sababu alikutana na Mungu. Mtu yeyote anayekutana Naye, na anamjua, na kuchukua Uzao wa

Ibrahimu, ataita chochote kinyume cha Neno la Mungu, kana kwamba ni uongo, yeye atalichukua Neno la Mungu kwanza.

56 Kisha tunamchukua mtu mwingine, Musa, nabii mtoro, huko nyuma kabisa upande wa nyuma ya jangwa, tumaini lote la kuwahi kuwakomboa watu wake kamwe, ambalo Mungu alimtuma kulitekeleza, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, hakuna ukombozi tena. Alikuwa ametulia, na kuoa mwanamke mrembo, alikuwa na m—mvulana mdogo. Naye alikuwa ameridhika vizuri, akijua ya kwamba siku moja angewarithi kondoo wote wa Yethro, na kadhalika, naye angeweza kuishi kwa amani huko nyuma ya Mlima Horebu.

57 Lakini siku moja kando ya kile kichaka aliona kijiti kikiwaka moto ambacho hakikuteketea. Mungu ana njia za ajabu za kuwavutia watoto Wake. Basi alipokanyaga mahali hapo, kulikuwa na Sauti iliyosema, "Vua viatu vyako, Musa, kwa kuwa mahali unaposimama ni patakatifu."

58 Ni tofauti ya jinsi gani iliyoleta ndani yake! Alikuwa ameogopa na kumtoroka Farao, kwa sababu alikuwa amemwua Mmisri. Lakini kesho yake, tunamwona huku mkewe ameketi juu ya nyumbu pamoja na mvulana mdogo nyongani mwake, masharubu yakining'inia chini, fimbo iliyopinda mkononi mwake, nywele zenye mvi zikipepea, umri wa miaka themanini, akishuka kwenda.

"Kwani unaenda wapi, Musa?"

59 "Nashuka kwenda Misri kuiteka." Uvamizi wa mtu mmoja. Mbona, hilo linasikika la kipuuzi, lakini uzuri wake, aliiteka, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu. Hakujali ilionekanaje, alikuwa amekutana na Mungu, naye alijua Mungu angeweza kutimiza Neno Lake. Alikutana na Mungu.

60 Kama hilo halikuwa tamasha la kuchekesha: mtu mmoja, huku mkewe amepanda nyumbu, mvulana mdogo kwenye nyonga yake, na maskini fimbo iliyopinda, masharubu yakipeperushwa namna *hiyo*, wakishuka kwenda kuteka taifa kama Urusi. Lakini haikuleta tofauti yoyote mradi Mungu alikuwa amekutana naye na kuliagiza, hilo tu ndilo jambo muhimu. Mungu anapokutuma, hilo latosha milele. Amina.

61 Mchukue maskini bikira Mariamu, msichana mdogo tu wa kawaida, huko Nazareti, maskini, mji mdogo katili ambamo uovu, karamu za usiku, na kadhalika, bali yeye alijiweka safi. Siku moja, akienda zake kwenye kisima cha mjini kuchota maji yake ya asubuhi, huenda alikuwa akitafakari ndoto fulani aliyokuwa ameota, ama Andiko fulani alilokuwa amesoma, labda Isaya 9:6, basi akienda zake huko ameshika mtungi wake wa maji chini ya mkono wake, akitembea asubuhi moja, ikatokea Nuru kuu iliyomulika mbele yake, na Malaika akasimama pale, kasema, "Salamu, Mariamu, umebarikiwa miongoni mwa wanawake. Umepata kibali kwa Mungu. Na

binamu yako Elisabeti, huko Uyahudi, amepita umri wa kuzaa, lakini nilikuwa huko siku chache, ndipo nikakutana na mumewe Zakaria, Mungu anatuma mtoto mchanga nyumbani mwao, yeye aliyeitwa tasa, sasa atakuwa mama. Nawe Mariamu, ulipata neema kwa Mungu. Nawe utampata Mtoto, Mwana, nawe utamwita Jina Lake YESU."

Akasema, "Mambo haya yanawezekanaje?"

62 Yeye akasema, "Roho Mtakatifu atakutia uvuli; Kitu hicho kitakatifu kitakachozaliwa kwako kitaitwa Mwana wa Mungu. Maana kwa Mungu hakuna lisilowezekana." Jinsi ilivyombadilisha maskini msichana huyo!

63 Sikilizeni, sote tungeweza kuchukua somo kutoka kwa Mariamu: Kamwe hakungojea mpaka alipohisi uhai, hakungojea chochote cha hakika, Neno lake lilimtosha, akaanza kwenda zake akishangilia, akisema, akishuhudia, atampata Mtoto huyo kabla ishara yoyote inayoonekana kutokea. Hivyo ndivyo mwaminio halisi anavyomwamini Mungu kwa Neno Lake, na kuanza kushuhudia, ukimsifu Mungu mara unapoweza kuridhika na ukweli kwamba Mungu alisema hivyo. Hilo ndilo linaloleta tofauti: Mungu alisema hivyo.

64 Hebu tumfuatilie kwa dakika chache wakati tukiwa naye. Anaingia Uyahudi, kisha anapanda mlimani. Naye Elisabeti alikuwa binamu yake, Yesu na Yohana walikuwa binamu wa pili. Basi Elisabeti alikuwa huko juu wakati huo, akiwa mja mzito wa miezi sita, lakini huyo mtoto mchanga hakuwa amesogea bado, hilo kwa jumla si la kawaida, mtu yeyote anajua hilo.

65 Elisabeti alikuwa amejificha. Labda alikuwa ameketi huko nyuma kwenye kibanda kidogo, akitengeneza vijiatu vidogo, na kadhalika, kwa ajili ya mtoto mchanga. Naye anaangalia nje ya mlango, anamwona maskini Mariamu, mrembo akija mbio, maskini mwanamwali huyo wa Kiyahudi, na upesi tu alivyoweza kuja. Ndipo akavuta pazia, naye akaona ya kwamba ilikuwa ni binamu yake mwenyewe. Loo, ninaweza kumwona akitoka nje mbio upesi awezavyo, akimshika Mariamu shingoni, na kuanza kumkumbatia na kumbusu.

66 Ninapenda, kuwaona wanawake wakifanya hivyo; ninapenda kuwaona wanaume wakipeana mkono mzuri, wa mtindo wa kale.

67 Hapa siku moja, nilikuwa pamoja na mke wangu katikati ya mji, mama fulani akasema, "Halo hapo, Dada Branham."

Ndipo nikamwambia, "Hivi—hivi hukuzungumza na mama huyo?"

Akasema, "Nilizungumza."

Nikasema, "Sikukusikia, nami nina hakika hakukusikia."

"Loo," akasema, "Ni—nilitabasamu."

Nami nikasema, “Sasa, Mpenzi, maskini tabasamu dogo, la kijinga halichukui mahali pa ‘U hali gani?’ ama kitu fulani.”

68 Loo, mwajua, watu ni baridi sana wao kwa wao siku hizi. Sisi ni ninii tu, siku hizi . . . Ilikuwa kwamba ungeweza kutoka nje, na—na mtu fulani akishikwa na ugonjwa, majirani wangeingia na kuwasaidia, walikuwa na ushirika halisi. Lakini siku hizi, hujui jirani yako amekufa, isipokuwa ulisome kwenye gazeti. Kuna *kitu kingine*, watu wanatengana sana. Tunahitaji ushirika. Mungu aturehemu.

69 Mariamu anakimbia na kumshika Elisabeti, huku Elisabeti akimshika Mariamu, basi wote wawili walikuwa wakikumbatiana kwa utamu na kuzungumza. Nami ninaweza kumsikia Elisabeti akisema, “Loo, Mariamu, sijawahi kukuona ukionekana mrembo hivyo. Macho yako yanametameta sana, na uso wa—wako ni mzuri sana. Unaonekana mwanamke wa kupendeza sana. Nadhani, labda, wewe na Yusufu bado mko pamoja?”

“Naam, bado tuko pamoja.”

Naye akasema, “Unajua, Mariamu, kwamba mimi ni mja mzito?”

“Naam, ninajua, ninajua. Nami ni mja mzito, pia,” akasema Marimu.

Naye akasema, “Loo, kumbe, wewe na Yusufu tayari mmeoana.”

“La, mimi na Yusufu hatujaoana.”

70 Ndipo sura ya mshangao mkubwa namna hiyo hapana shaka ilikuja kwenye uso wa Elisabeti, “Unataka kusema kwamba wewe ni mja mzito, huku wewe na Yusufu hamjafunga ndoa?”

“Hiyo ni kweli.” Loo, na hilo tabasamu usoni mwake!

“Mariamu, kuna nini?”

71 Mnaona, alikuwa amekutana na Mungu, hilo lilileta tofauti. Jambo fulani lilikuwa likitukia. “Loo,” akasema, “jinsi nilivyojua ya kwamba ulikuwa mja mzito, kulikuwa na Malaika aliyekutana nami jana asubuhi, nilipokuwa nikienda kisimani. Naye akaniamkua vizuri sana, na kuniambia nimepata neema kwa Mungu, na Roho Mtakatifu atanitia uvuli, akaniambia ya kwamba nitapata Mwana. Halafu akasema ya kwamba wewe utapata mwana, pia.”

Akasema, “Lakini mpenzi, huyo mtoto amekufa. Nimekuwa na mimba kwa muda wa miezi sita, wala huyo mtoto hajasogea bado.”

72 Akasema, “Loo, nisingehofia hilo. Unajua wakati aliposema ya kwamba Roho Mtakatifu angenitia uvuli, na huyo Mtoto mchanga ambaye angezaliwa ndani yangu, kutoka kwangu,

angeitwa Mwana wa Mungu, nami ningemwita Jina Lake YESU."

73 Na mara tu aliposema, "YESU," mara ya kwanza Neno hilo lilipopata kutoka kwenye mdomo wa mwanadamu, mtoto Yohana akampokea Roho Mtakatifu, amekufa tumboni mwa mama yake, na akaanza kuruka kwa shangwe katika tumbo la uzazi la mama yake.

74 Loo, kama Jina la Yesu Kristo lingemfufua mtoto aliyekufa na kumjaza na Roho Mtakatifu, linapaswa kufanya nini kwa kanisa lililozaliwa mara ya pili linalodai kuwa limejaa Roho Mtakatifu?

75 Ninii. . . "Mara kuninii kwako. . . " Kasema, "Heri wewe," kasema, "kwa maana kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu. . . Mama ya Bwana wangu amenijiliaje? Mara niliposikia Jina Lake, kitoto changu kichanga kiliruka tumboni kwa shangwe." Yohana alianza kupaza sauti aliposikia Jina la Yesu Kristo likitamkwa, akafufuka.

76 Tangu wakati huo, hapakuwapo na wasiwasi wowote kuhusu huyo mtoto, tena, kwa sababu walijua angekuwapo. Mambo makuu ya Mungu yalikuwa njiani.

77 Simoni, yule mvuvi, mwenye shaka, mwenye kudhihaki, kwa Andrea ndugu yake kuhusu Yesu kuwa Masihi, wakati mmoja, Andrea alimshawishi aje mkutanoni, na mara alipokuja Mbele za Mungu, alimwangalia, na kusema, "Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona." Na tangu wakati huo, Petro alikuwa mwaminio.

78 Ilikuwa ni yule Paulo Mtakatifu mashuhuri ambaye kwanza alikuwa Sauli, mtesi wa Kanisa, akienda zake Dameski akiwa na barua mifukoni mwake kutoka kwa kuhani mkuu kuwachukua watu hao wote waliokuwa wakipiga makelele na kunena kwa lugha, na kadhalika, na kuwatia gerezani. Yapata adhuhuri, kulikuwa na Nuru iliyoangaza kutoka Mbinguni, naye akaanguka kwa miguu yake mavumbini. Ndipo ikaja Sauti ikisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?" Na tangu wakati huo, Sauli alibadilishwa akawa Paulo na akawa mwaminio halisi, na mtenda kazi Kanisani.

79 Ilikuwa pia katika ibada yetu jana usiku, wakati maskini ombaomba kipofu, ambaye hata hakuwa na chakula nyumbani mwake, labda, aliketi kando ya barabara, akiomba, kipofu, asingeweza kutofautisha mwanga wa mchana na giza, bali alikuja Mbele za Bwana Yesu. Aliita mpaka imani yake ikamgusa Yeye, na tangu wakati huo angeweza kuona. Alipomgusa Mungu, tangu wakati huo maisha yake yalibadilika.

80 Kulikuwako na mwenye ukoma, amelala langoni, akilia, "Ni najisi, ni najisi!" Naye Yesu akapita, ndipo alipokutana na Yesu kwa mara ya kwanza, Yeye alimgusa, na tangu wakati huo ukoma ukaisha.

81 Ilikuwa ni yule mwendawazimu huko Gadara, ambaye alikuwa na nguvu sana amepagawa na ibilisi, hata wangemfunga kwa minyororo, naye angeivunja ile minyororo, na kujikatakata kwa vipande vya mawe, alikuwa ni mtu mbaya sana hata hakuna mtu angaliweza kupita, angewaua kama angeweza kuwashika, wamepagawa sana na ibilisi. Kila mtu aliikwepa hiyo njia. Siku moja Yesu akaja, na tangu wakati huo alikuwa mtu aliyebadilika, naye alikuwa na akili timamu, naye angeweza kwenda nyumbani kwa familia yake. Tangu wakati huo, alikuwa amekutana na Mungu.

82 Ilikuwa ni yule mwanamke kisimani, jinsi ambavyo dhambi zake zilikuwa mbaya sana hata asingeweza kuja kisimani wakati wa kawaida wa mchana, ilimbidi kungojea mpaka wanawake wote wenye heshima walipoondoka kisimani. Hakuna mtu mjini angemsikiliza, kwa sababu alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Siku moja, wakati alipokuwa amesimama pale kwenye kisima cha Yakobo nje ya mji wa Samaria, aliangalia, naye akamwona Mtu fulani pale ameketi ukutani aliyesema, “Nipe maji ninywe.”

Naye akamwambia, “Si kawaida kwa Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho.”

83 Akasema, “Lakini kama unajua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” Mazungumzo yakaendelea kwa muda. Baada ya kitambo kidogo, akapata shida yake ilipokuwa, Naye akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Hiyo ni kweli. Una watano, na yule unayeishi naye siye mume wako.”

84 Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii. Musa ametwambia ya kwamba Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii kama alivyo yeye. Naye Masihi ajapo, Yeye atatuambia mambo haya.”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

85 Jambo fulani likampata, tangu wakati huo, alikuwa mjini akitoa ushuhuda, “Njoni mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Mambo yalikuwa yamebadilika alipokutana na Mungu.

86 Siku moja, Mungu ambaye ni uzima, uzima na mauti vilikutana. Mauti daima yalimtilia shaka kuwa ni Mwana wa Mungu. Wakati ibilisi alipokuwa Naye huko nje, alimjaribu, kasema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate, nitakuamini.” Alijaribiwa.

87 Alishangaa tu kwamba Huyo alikuwa ni nani, “Je, huyo alikuwa ni nabii, ama kweli huyo alikuwa ni Mungu?” Hakujua.

Hakujua wakati huo kwamba ilibidi Mungu afanyike mwili na kukaa miongoni mwetu.

88 Siku moja askari wa Kirumi alimfunga kitambaa usoni, akachukua mwanzi na kumpiga kichwani, na kusema, "Sasa, basi kama wewe ni nabii, kama wewe ndiye nabii huyu, tuambie ni nani aliyekupiga."

89 Hata hivyo, Yeye asingeweza kujibu, kwa sababu angekuwa akimjali ibilisi.

90 Msalabani walimwuliza, "Shuka msalabani, tutakuamini kuwa wewe ni Mwana wa Mungu." Majaribu hayo yote, ibilisi hakujua huyo aliyekuwa katika mwili huo wa nyama alikuwa ni Nani. Kwa hiyo akipanda kilimani kwenda Kalvari, Shetani bado hakuridhika kwamba Huyo alikuwa ni Mungu, Imanueli, Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira.

91 Hebu tufunge safari ya kwenda Yerusalemu kwa muda kidogo. Ni kwenye asubuhi mbaya sana, jua linaonekana la kuchekesha. Wakati dhabihu ya asubuhi ilipotolewa, moshi kutoka kwenye madhabahu ya shaba, badala ya kupanda juu kwa Mungu, Yeye aliikataa. Ulikuwa umetanda juu ya mji, ulikuwa ni wakati wa huzuni.

92 Tumesimama katika chumba cha juu. Nasikia kelele, kumekuwako na ghasia huko chini katika ukumbi wa hukumu wa Pilato tangu alfajiri na mapema, yapata saa tisa, kumekuwako na ghasia kule chini. Ni kitu gani? Hebu twende dirishani, nasikia kelele. Hebu vuteni mapazia nyuma. Ninasikia kitu fulani kikigongagonga barabarani unapotoka kuelekea Golgotha.

93 Huyu hapa Mtu akishuka mtaani, msalaba wa kale, unaoparuza mabegani Mwake, ameubeba, akiukokota mgongoni, ukigongagonga juu ya hayo mawe magumu, ukiparuza mahali hapo, nyama zimetoka mabegani Mwake, taji ya miiba kichwani Mwake, iliyochanganyikana na machozi na damu ikitiririka usoni Mwake, kwa dhihaka, mate ya askari yamejaa kwenye ndevu Zake, huku uso Wake ukitokwa na damu ambapo waling'oa makonzi ya ndevu kutoka usoni Mwake. Msalaba wa kale ukikokota nyayo zilizojaa damu, wakati akitembea barabarani.

94 Ninaona mgongoni Mwake, Yeye ana joho mabegani Mwake, lililofumwa kote bila mshono, kuna madoa madogo mekundu kote kwenye koti hilo. Anapopanda kilimani, hayo madoa yanazidi kuwa makubwa zaidi, na makubwa zaidi, na makubwa zaidi, yakienea, baada ya kitambo kidogo, yote yanakuwa doa moja kubwa mno.

95 Nyuki wa mauti anashuka, na kuanza kuvuma karibu Naye, akivuma, "Nimempata sasa, akienda zake Kalvari. Nitampata kule juu, na huo utakuwa ndio mwisho wa kitu hiki kinachoitwa Masihi."

96 Nyuki huyo wa mauti, humchoma kila mtu. Lakini, kama nyuki mwingine yeyote, kama nyuki huyo akiwahi kuchoma kwa kilindi vya kutosha, atapoteza mwiba wake. Mdudu yeyote ama nyuki, kama akiwahi kuchoma kwa kilindi sana, hawezi kuchoma tena. Asingeweza kuchoma kwa kilindi vya kutosha katika damu ya mwanadamu, lakini ndugu, dada, wakati alipochomeka mwiba wake ndani ya Mwana wa Mungu, huo mwiba uling'oka kutoka . . .?. . .

97 Si ajabu mtu angeweza kusimama na kusema, "Ee mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?" Kifo kilipokutana na Mungu, kilipoteza mwiba wake, hakiwezi kumchoma Mkristo tena. Kinaweza kulia na kupiga kelele, lakini kimepoteza mwiba wake. Nina furaha sana! Nina shukrani sana usiku wa leo kuwa Mkristo, kujua ya kwamba mauti hayana mwiba wowote, tena. Yanaweza kuvuma, na kupiga kelele, na kujaribu kututisha, bali tunajua ya kwamba mwiba ulikuwa umechomelewa mwilini Mwake, na tangu wakati huo, Mungu alichomoa mwiba kutoka katika mauti, na leo hii, mauti hayana mwiba.

98 Loo, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Mnaamini hilo? Mnakubali hilo kuwa . . .?

99 Wakati mmoja mimi, mwenyewe, nikiwa nimelala kwenye kitanda cha hospitalini, mvulana mdogo wa Kiairishi, nimelala pale nikifa, baba yangu akilia, maskini nesi amesimama pale, na moyo wangu ukidunda tu mara kumi na saba kwa dakika moja, mgao mkubwa wa nusukaputi ulikuwa umeingia moyoni mwangu kutokana na upasuaji wa sehemu ya uti wa mgongo. Ndipo daktari akasema, "Hakuna njia kwake kuishi," nami nikasikia hilo. Nao wakavuta pazia karibu nami.

100 Ndipo nikasikia Sauti ikiingia, kama vile kelele zikija kama majani yanayovuma, nikawaza, "Jambo ndilo hili. Mungu, siwezi kukupa maisha yangu namna hii, kama waridi la kale linaloangusha petali." Nikasema, "Bwana, sijui jinsi ya kuomba, bali nimeambiwa ya kwamba Wewe ni Daktari mkuu, juu ya madaktari wote. Kama utanijalia tu kuishi, kamwe sitakuonea aibu tena, nitapiga mayowe juu ya nyumba, kutoka pembeni mwa barabara." Basi kuanzia saa hiyo, nikaanza kuishi, nami nimeishi tangu wakati huo.

101 Na siku hizi, baada ya miaka thelathini na mmoja, nina furaha kuwa nimesimama nyuma ya mimbara usiku wa leo kusema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," kwa sababu siku moja nilikutana na Mungu.

102 Kila mmoja wenu ana tukio kama hilo. Upo wakati ambapo mtu analetwa uso kwa uso, kukutana na Mungu, kumkubali, ama kuachana Naye. Huenda huo ukawa ndio wakati wako

usiku wa leo, bwana, huenda ikawa usiku wa leo ndio wakati wako, mama, kwamba itakubidi, usiku wa leo, kumpokea au kumwacha aende.

103 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu sasa, tunapotafakari juu ya maneno haya.

104 Sijui, humu jengoni usiku wa leo, kwenye roshani upande wangu wa kulia, kungekuwa na mtu huko juu kwenye roshani hii upande wangu wa kulia, wangeinua mikono yao, na kusema, "Mungu, tangu wakati huu, nimeishi maisha vuguvugu ya Kikristo," ama labda, "Sijakukubali Wewe hata kidogo, lakini tangu wakati huu, nitakukubali Wewe kama Mwokozi wangu"? Waweza kuinua mkono wako? Roshani upande wangu wa kulia, mtu yeyote huko juu ambaye si Mkristo, angesema, "Tangu wakati huu, nitampokea Bwana Yesu"?

105 Roshani huko nyuma, mtu fulani huko juu inua mkono wako, useme, "Mimi si Mkristo, Ndugu Branham, lakini ninataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu"? Roshani upande wangu wa kushoto, waweza kuinua mkono wako hapo juu, mahali fulani, na kusema, "Ninataka kumkubali Kristo"? Chini kwenye orofa ya chini upande wangu wa kushoto, mtu fulani inua mkono wako, ukisema, "Ninataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu, tangu wakati huu, ninataka kuwa Mkristo." Marefu ya katikati hapa, mtu fulani inua mkono wako, useme, "Ninataka kumkubali Kristo." Roshani upande wangu wa kulia, kuna mmoja ambaye ungeinua mkono wako, na kusema, "Ninataka kumkubali Kristo"?

106 Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo, hilo ni zuri sana. Mvulana mmoja mdogo, yapata umri wa miaka kumi na miwili, kumi na minne kutoka kwenye nyumba nzima ya watu. Sijui kama ni kwa sababu ninyi nyote ni Wakristo na tayari mmemkubali Yeye. Kama sivyo, ungekuwa wa namna hiyo kumwinulia mkono wako, na kusema, "Tangu wakati huu, nitakutolea ahadi hii, Bwana, ninajisikia ya kwamba ninapaswa kuwa mtumishi Wako, nitakuinulia Wewe mkono wangu"? Kuna mmoja, mbali na mvulana huyu mdogo?

107 Mungu akubariki, hapa, bwana. Hilo ni jema. Fanya uamuzi wako sasa. "Na tangu wakati huo." Kuna wengine hapa wanaoweza kukumbuka ya kwamba wakati mmoja ulikuwa na ujuzi mzuri wa Kikristo, lakini jambo fulani likatukia? Jambo fulani lilitukia, na tangu wakati huo hujajisikia sawa tokea wakati huo. Waweza kuinua mkono, useme, "Niombee"?

108 Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni—hiyo ni kweli. Kwenye roshani, "Tangu wakati huo, mimi . . . " Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Popote pale, Mungu akubariki. Naam, hilo ni zuri. Hakika nitawaombea. Mungu akubariki.

109 Sasa huko chini kwenye orofa ya chini, inua mkono wako, useme, "Wakati mmoja nilipata tukio tamu, Ndugu Branham,

lakini jambo fulani likatukia siku moja, na tangu wakati huo, sijajisikia karibu na Mungu tokea wakati huo." Inueni mikono yenu. Mungu awabariki. Hilo ni jema. Anajua moyo mwaminifu. Bila shaka, Yeye anajua.

110 Jambo ndilo hilo. Ninaangalia, ninangojea. Endeleeni tu kuomba, kila mtu huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa. Ninamwangalia mtu fulani. Endeleeni tu kuomba, endelea kuinamisha kichwa chako. "Tangu wakati huo . . . " Loo, Bwana awe pamoja nanyi.

111 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya huyu kijana mwanamume aliyeinua mkono wake usiku wa leo, naye anataka kuwa Mkristo. Jalia hii iwe ndiyo saa, Bwana, ambapo utampokea katika Ufalme Wako. Naomba, tangu saa hii, anaweza kusema katika miaka ijayo, endapo kuna mwaka ujao, "Nilikuwa huko chini kwenye jumba la mikutano usiku mmoja, Kitu fulani kisicho cha kawaida kikanena na moyo wangu, na tangu wakati huo." Ninaomba Wewe utamfanya mmishenari, Baba, kukiwapo na kesho ya umishenari. Naye atawaendea watu, na ushuhuda wake ungekuwa, "Na tangu usiku huo na kuendelea . . . "

112 Wengi wa hawa wa thamani wanaoinua mikono yao, kwamba wakati mmoja walikuwa wamekupenda, na kukuamini Wewe, nao wakawa na tukio zuri sana, lakini kitu fulani kiliyatatiza maisha yao, tangu wakati huo na kuendelea, hawajajisikia vizuri kabisa, Mungu wa Mbinguni, lifanye usiku wa leo, kwamba tangu usiku huu na kuendelea, watajisikia tofauti kulihusu. Tujalie, Bwana. Jalia wampokee Kristo tena, kwa utamu, kwa unyenyekevu, moyoni mwao usiku wa leo. Baba Mungu, tujalie. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

113 Hebu tuimbe wimbo wetu mdogo sasa. Hatujui yale Roho Mtakatifu atakayofanya. Kwenye wimbo wetu mzuri wa kale sasa, *Nampenda*, hebu tufanye ninii . . . mkipenda. "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Sisi sote pamoja sasa, tunapomwabudu katika wimbo.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

Ni wangapi walio Wakristo sasa, ambao kweli wanampenda? Mwinulie Yeye mkono.

> Na- . . .

Funga tu macho yako na uuimbe.

> . . . Nampenda,
> Kwani . . .
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

114 Loo, Yeye si ni wa ajabu? Hivi hujisikii vizuri sana moyoni mwako? Umesuguliwa tu kabisa, ukiwazia, "Tangu wakati huo. . ."

115 Ninakumbuka, huko nyuma kwenye kibanda kidogo cha makaa ya mawe, usiku mmoja, nilikuwa na njaa sana ya Mungu. Nikashuka kwenye kanisa langu la Kibaptisti, naye mchungaji akasema, "Njoo huku, Billy, nipe mkono wako wa kuume, ligeukie kusanyiko na kuwaambia u—unamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Wewe ni mvulana mzuri." Hilo halikulitatua.

116 Nikashuka kwenye Kanisa dogo la Waadventista wa sabato, nao wakaniambia inanibidi kuadhimisha siku ya Sabato, wala nisile nyama, na kadhalika. Ndipo mimi. . .Hilo halikuridhisha.

117 Nikarudi, nikachukua gunia kuukuu, nikaingia kwenye kibanda, nikapiga magoti pale, na, loo, jamani, tangu wakati huo, jambo fulani lilitukia. Tangu wakati huo, ninakumbuka, kulikuwa na amani tamu iliyokuja nafsini mwangu ambayo, loo, ilimaanisha mengi sana kwangu. Mnajua Yesu yuyo huyo yuko hapa usiku wa leo. Yeye anatupenda, hivi hamwamini hilo?

118 Sasa, hatujasambaza kadi zozote za maombi, kama nilivyosema, kwa siku chache zilizopita usiku, lakini kama msimamo wangu, na Wakristo wote wanaamini hili, ambao kweli wamezaliwa mara ya pili, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo?

119 Nilikuwa nikijaribu usiku wa leo, juu ya jambo lingine kuona kama wenye dhambi, ningeweza kuwapata. Kumbukeni, uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo, kamwe hutalifanya kubwa jambo dogo, huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo nilifikiri labda kulikuwa na kundi la wenye dhambi ambalo lingekuwa karibu, nami ningeweza kuwaalika waje kumpokea Bwana Yesu.

120 Ndugu du Plessis kwa kawaida ndiye hufanya wito wa madhabahuni. Hivi majuzi usiku nilifanyiza mmoja, wachache walikuja, lakini inaonekana kana kwamba karibu wote ni Wakristo.

121 Mnachohitaji huku Oklahoma, nionavyo huku, ni uamsho mzuri tu, wa mtindo wa kale. Mna nyenzo za kufanyia hilo, mna watu mashuhuri hapa mjini. Ni nani aliye mkuu zaidi hudumani kuliko Tommy Osborn, Ndugu Oral Roberts? Baadhi ya watu mashuhuri sana ulimwenguni, wametia nanga mumu humu mjini mwenu. Huku kunapaswa kuwa ni mahali pa kiroho sana kuliko pote ulimwenguni, mumu humu ambamo Abundant Life, na—na *Faith Digest*, na hayo magazeti makubwa, na kadhalika yanayoenezwa kote ulimwenguni, kila mahali. Huku kunapaswa kuwa, ninii tu, kama tu sega la asali ambapo nyuki huingia ndani na kutoka, wakileta asali, kunapaswa kuwa.

122 Kile Oklahoma inachohitaji hapa sasa, ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale, kuibuka. Makanisa yetu yameuendea

ulimwengu kupita kiasi, magumu kupita kiasi, ya kiakili kupita kiasi, mitindo mingi—mingi tu kupita kiasi. Tunahitaji Injili ya Kipentekoste ya mtindo wa kale, na uamsho wa kale wa Kipentekoste, mikutano ya maombi ya usiku kucha, na hayo ndiyo tunayohitaji, enyi marafiki. Kumrudia Mungu, ambapo kanisa linaweza kupokea baraka zake na kupokea ninii yake . . .

123 Sasa, mambo hayo, wafuasi wanaongezeka katika madhehebu yenu. Ninathamini hilo, kila mmoja wenu, ninathamini hilo kwa moyo wangu wote, nimeweka kila kitu nilichoweza kwake.

124 Nilipokuja kutoka kwa kanisa la Kibaptisti kwa mara ya kwanza, niliona, nilipokutana na Pentekoste, niliwazia, "Hili ndilo." Ndipo nikaja kugundua walikuwa wamegawanyika katika madhehebu mbalimbali, sawasawa na Wabaptisti. Mmoja alisema, "Njoo, uende pamoja nasi." Huyo mwingine akasema, "Njoo, uende pamoja nasi," lakini nimesimama moja kwa moja katika pengo, na kuwakumbatia wote, nasema, "Sisi ni ndugu."

125 Sisi ni ndugu, hivyo ndivyo tulivyo, marafiki. "Hatujagawanyika, sisi sote ni Mwili mmoja." Hiyo ni kweli. "Hima twendeni mbele askari Wakristo." Tunapaswa kuwa katika maombi, daima tukikutazamia Kuja kwa Bwana, kwa kuwa tunaamini Yeye atakuja hivi karibuni.

126 Sasa, kama Yesu angekuwa hapa, usiku wa leo, katika umbo linaloonekana, basi ingekuwa ni kosa. Kama Yesu Kristo angesimama kwenye mimbara hii usiku wa leo, Yesu Kristo wa Mbinguni, angesimama kwenye mimbara hii usiku wa leo na kudai kuwa ni Yesu Kristo, angekuwa ni mpinga-Kristo, angekuwa hivyo hasa, kwa kuwa wakati Yesu atakapokuja, Unyakuo unatukia. "Kama vile nuru itokavyo mashariki hata magharibi, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu. Kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri."

127 Lakini Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani Yake yuko hapa usiku wa leo. Yeye yupo hapa usiku wa leo katika Kanisa Lake, "Walipo wawili watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu." Tumeyapitia hayo, na kuyapitia tena. Nao Uwepo Wake upo hapa.

128 Na kile—kile kinachonitikisa, rafiki, Ndugu David ameketi hapa, huko Afrika Kusini, huko Durban, wakati hao wenyeji wanaovaa blanketi, maelfu yao . . . Hapo waliketi Waislamu kwa maelfu, dini zote za namna mbalimbali, na, ambazo hukuziwazia kamwe. Nilimwuliza Sidney Smith, nafikiri huyo ndiye . . . Huyo ndiye meya? Sidney Smith, Durban. Meya wa Durban, tulikuwa tukitoka, akasema, "Ndugu Branham, Afrika haijawahi kuwa na kitu kama hiki," tukielekea uwanjani.

129 Basi kulikuwa na mtu aliyekuwa na kibandiko juu yake, amebeba sanamu. Nami nikasema, “Kibandiko hicho ni cha nini?”

Kasema, “Yeye ni Mkristo.”

Nikasema, “Na anabeba hiyo sanamu?”

Akasema, “Yeye ni Mbasoto.” Ninaamini ndivyo. Mbasoto, kitu kama hicho. Mzulu.

Kasema, “Ninaweza . . . ” Kasema, “Ninaweza kuzungumza lugha yake. Ongea naye, mwite chochote utakacho.”

130 Ndipo nikaongea naye, nikasema, “Kwa nini unaibeba sanamu hiyo? Hivi humwamini Mungu?” Aliamini, naamini aliita *Amoya*, kitu kama hicho, “upepo, nguvu zisizoonekana.” Alimwamini Amoya, lakini siku moja, baba yake alikuwa amebeba sanamu hiyo, naye simba akamfukuza, naye akawasha moto mdogo, ndi—ndipo huyo simba akatoroka, kwa hiyo sanamu hii ilikuwa ni Mungu, pia. Sasa, huo si Ukristo, huo si Ukristo, la, bwana.

131 Ndipo nikasema, “Bwana, mimi mwenyewe ni mwindaji. Huo moto ndio uliomfukuza huyo simba, hiyo sanamu haikuwa na uhusiano wowote naye, moto ndio uliomwogopesha huyo si—simba.”

132 “Ah,” angeibeba, kwa vyovyote vile, kwa hiyo, “kwa usalama. Kama Amoya, yule Mungu asiyeonekana alishindwa, *huyu* hatashindwa.” Sasa, hizo—hizo wakati mwingine huitwa nguvu za Ukristo katika milki nyingi. Ni vibaya sana.

133 Lakini kwenye siku niliyowapa ile hadithi rahisi, “Kama Yesu Kristo, ambaye amenenwa katika Biblia, kama Yeye atakuja hapa na kufanya jambo lile lile alilofanya, kama Yeye atafanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa duniani kuwathibitishia watu Yeye alikuwa Ndiye Masihi . . . ”

134 Walijuaje Yeye alikuwa ni Masihi? Myahudi alijuaje? Myahudi halisi, walipomwona . . . Nathanaeli alimjia. Akasema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.”

Kasema, “Rabi, ulinijua lini Wewe? Hujawahi kuniona maishani Mwako.”

Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

135 Akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Huyo alikuwa ni Myahudi halisi, mteule, aliyechaguliwa tangu zamani kwa Uzima wa Milele.

136 Kulikuwako na baadhi ya makuhani, wamesimama pale, wakasema, “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli.”

137 Yesu akasema, “Mkisema hayo dhidi Yangu, nitawasamehe; lakini siku moja, Roho Mtakatifu atakuja na kufanya hayo,

neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe." Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa watu.

138 Hivyo ndivyo yule mwanamke kule Samaria alivyojua ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, kwa kuwa Yeye alimwambia mawazo yaliyokuwa moyoni mwake, kwa kuwa Musa alisema Masihi angekuwa Mungu-Nabii.

139 Sasa, kama Yeye angesimama hapa usiku wa leo, amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kukuponya, kwa sababu tayari amekuponya; asingeweza kusamehe dhambi zako, tayari amezisamehe. Uponyaji na wokovu ni kazi iliyomalizika ambayo tayari imekamilika wakati Yesu alipokufa pale Kalvari. "*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Hiyo ndiyo Injili kama ninaijua.

140 "Imani chanzo chake ni kusikia. Ndipo Mungu ameweka kanisani mitume, manabii, wainjilisti, waalimu, na wachungaji, wote kwa ajili ya ukamilifu wa watakatifu." Sasa, kama Yeye anaweza kuushika moyo wako, basi anaweza kutenda kazi Zake, lakini, mradi tu unaweza kujiondoa njiani, mradi tu unaweza kujituliza, na kumwacha Roho Mtakatifu achukue mamlaka. Yeye alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Nalo ja—jani halininii . . . Mzabibu hauzai tunda, bali unalipa tawi nguvu lipate kuzaa matunda. Sasa, ungezaa tunda la aina gani? Aina ya uhai uliokuwa katika huo mzabibu. Vema, hilo ndilo jambo lile lile Kanisa lifanyalo.

141 Leo, kama unataka kupata—kama unataka kupata zabibu, nenda kwenye shamba la mizabibu; kama unataka kupata maboga, nenda kwenye mmea wa maboga. Lakini jambo ni kwamba siku hizi, watu huja makanisani na kukuta theolojia kavu, iliyokatwakatwa, hawana Roho hata kidogo. Tunachohitaji leo, ni uamsho wa Roho wa Mungu miongoni mwetu kuturudishia, Mungu wa kweli na aliye hai.

142 Sasa, kama utafanya kama yule mwanamke alivyofanya . . . Sasa, nijuavyo mimi, hakuna mtu katika kusanyiko hili ninayemjua, isipokuwa ingekuwa ni Pat Tyler, aliyeketi papo hapo, na Ndugu Gene aliyeketi papa hapa. Hao ndio watu pekee ninaowajua katika kusanyiko hili.

143 Kama wewe—kama unaamini ya kwamba Yesu Kristo alikufa, akafufuka tena, akapaa Juu, katika mkono wa kuume wa Ukuu, umeketi mwili Wake, Roho Wake akarudi Kanisani kama tulivyokuwa tukifundisha, basi Yeye asipolitimiza Neno Lake, basi Yeye hakuwa Mwana wa Mungu; kama Yeye akilitimiza Neno Lake, basi Yeye yu hai. Baada ya miaka elfu moja mia tisa, Yeye angali hai.

144 Sasa, jambo ni kwamba, hivi atafanya hivyo? Kama Yeye aliahidi jambo hilo, Naye ni Mungu, hana budi kulitimiza. Anawajibika kwa Neno Lake, wala Yeye si bora kuliko Neno Lake. Wala mimi si bora kuliko neno langu, nawe ni bora kuliko

neno lako, Mungu si bora kuliko Neno Lake. Kama hatalitimiza, basi Yeye si Mungu; kama kweli akilitimiza, inathibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

145 Sasa, ninyi wagonjwa huko nje, kama mnaamini hilo, na mna imani ya kumgusa jinsi yule mwanamke alivyofanya . . . Je, Biblia inasema ya kwamba Yeye, sasa hivi, ni kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Je, Biblia inasema hivyo? Vema. Basi kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetendaje? Vile vile alivyotenda wakati ule. Hiyo ni kweli?

146 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu na kuomba. Nanyi ombeni ya kwamba Mungu ataninii . . . mtaweza kugusa ninii Yake, upindo, tuseme, wa vazi Lake. Sasa, endeleeni tu kuomba, nitaomba. Na kila mtu awe kimya kabisa. Nitawaomba kama watazima feni, kama watazima, kwa dakika chache tu. Sasa iweni na kicho kabisa na mwe katika maombi. Sasa huu ni wakati muhimu sana.

147 Nina hakika ya kwamba kila Mkristo angeweza kuthamini mahali ninaposimama sasa hivi. Mambo ambayo nimesema na nimekuwa nikizungumzia, ama ni ya kweli au si ya kweli. Sasa, iweni tu na kicho na mwombe, na kila mtu abaki kitini mwake. Haidhuru uko wapi, endelea tu kuomba, ukiamini kwa moyo wako wote.

148 Sasa, Baba, mkutano huu, Neno moja kutoka Kwako lingekuwa zaidi ya yale mtu yeyote angeweza kusema maishani, Neno moja tu ili watu hawa waweze kutoka hapa usiku wa leo, na kusema, "tangu wakati huo," hebu waseme hivi, kama Bartimayo kipofu, katika somo letu jana jioni, alimgusa Yesu na kumsimamisha, yule mwanamke aliyetokwa na damu alimgusa na kumsimamisha. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

149 Bwana, jalia watu hawa wamguse. Tuma neema Yako igusayo, Bwana, wapate kukugusa Wewe kwa ajili ya udhaifu wao, ili ulimwengu upate kujua ya kwamba Wewe ni wa kweli, na Wewe—Wewe ni Mwana wa Mungu, Nimewaambia kweli ya Neno Lako. Tujalie, kupitia Jina la Yesu Kristo.

150 Sasa, ombeni tu, na kusema, "Bwana Mungu, Ndugu Branham ni mwanadamu, yeye hanijui mimi." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

151 Na, bila shaka, nyote mnajua yale maono makuu yaliyotolewa, yaliyosemwa, hakuna hata wakati mmoja ambapo moja lilishindwa. Ono la kwanza lililokuja, nilikuwa na umri wa miezi kumi na minane.

152 Sasa, kama mtakuwa na kicho kabisa, Roho Mtakatifu ameanza kuingia chumbani.

153 Ninaangalia sasa upande wangu wa kushoto, kutoka kwangu. Ninamwona mtu akiomba, hiyo Nuru iko juu yake.

Ameketi upande wangu wa kushoto mwishoni mwa safu huko nje. Ana henia, ana shida ya pua, na yabisi kavu. Naye anaomba apate ukombozi. Unaamini, bwana, ya kwamba imani yako imegusa vazi Lake sasa, nawe unataka kuponywa? Utaukubali? Ikiwa utaukubali, inua tu mkono wako, useme, "Ninaukubali." Ameketi papa hapa nyuma upande wangu wa kushoto, mikono juu ya uso wako pale, ukiomba. Vema.

154 Kuna mtu papo hapo nyuma yake, anayeomba pia, bali yeye hajiombei mwenyewe, anamwombea msichana wake mdogo pale. Maskini msichana huyo ana shinikizo la chini la damu. Mke wako aliyeketi karibu nawe, pia, ana shida na viungo vyake, sivyo? Unaamini ya kwamba Mungu ataviponya? Unaamini? Inua mkono wako basi, useme, "Nitalikubali," naye Mungu atawapa afya. Mungu awabariki.

155 Vema. Nyuma hapa kwenye marefu haya ya katikati, mtu fulani hapa chini aamini, na Bwana na atujalie baraka. Sasa hapa, papa hapa katikati ya haya marefu, upande wa nje, mkono wangu wa kulia, kuna mwanamke aliyeketi pale, ana shida ya tezi anayoombea. Ili kwamba upate kujua mimi ni nani, ni nani ninaye—ninayemzungumzia, una mume nyumbani unayemwombea, naye ana ngiri. Unaamini ya kwamba Mungu atamponya? Unaamini, dada? Inua mkono wako kama utaukubali kwa moyo wako wote. Unaamini? Vema.

156 Huyu hapa mwanamke ameketi papa hapa kutoka kwangu, kwenye marefu ya kanisa, anaomba. Anamwombea mwanawe. Mwanawe yuko katika kitanda cha maradhi. Hayuko hapa, hata hayuko katika jimbo hili, yuko Arkansas. Ninii Yake . . . Yeye ni mlevi sugu. Bibi Kelly, huyo ndiye ninayeongea naye. Unaamini, Bibi Kelly? Simama kwa miguu yako, simama, simama, Bibi Kelly. Sasa, sikujui. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hiyo ni kweli? Sasa, sasa nenda zako ukamkute jinsi ulivyoamini. Mungu akubariki.

157 Kama mnaamini, enyi marafiki! Iweni tu na imani. Je, mnamwamini Mungu sasa? Iweni na imani sasa, amini tu kwa moyo wako wote.

158 Huyu hapa mtu ameketi papa hapa chini, moja kwa moja kwenye mkono wangu wa kulia tena, ameketi hapa mwisho. Ana shida ya mapafu, ni mahututi sana. Unatambua ya kwamba hiyo ni kansa, bwana, kwenye mapafu yako? Sikujui. Hiyo ni kweli?

159 Kama watu wanataka kuinua kichwa chao, ni sawa, sijali wakati wewe . . . ninapozungumza na mtu fulani.

160 Hatufahamiani, hiyo ni kweli, bwana? Sikujui wewe. Unaamini ya kwamba Mungu angekuponya na kukupa afya? Una kansa kwenye pafu. Wewe ni mhudumu, pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni . . . Wewe ni mhudumu wa Assemblies of God. Na mimi sikujui. Unaamini ya kwamba Mungu anajua wewe ni nani? Unaamini Yeye angeweza kuniambia wewe ni nani?

Je, ungeamini. . .kukufanya uamini sasa? Kwa sababu huna budi kuamini, la sivyo utakufa. Kasisi Lee Hildreth, hilo ndilo jina lako. Hiyo si ni kweli? Inua mkono wako. Vema. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Roho Mtakatifu, Yeye anataka kuyaokoa maisha yako, bwana. Amini kwa moyo wako wote.

161 Mnaamini sasa, ninyi nyote, kwa moyo wenu wote, yote yaliyo ndani yenu? Kila mahali, mnaamini? Mtu mwingine anataka kuamini?

162 Hapa, ninamwona mhudumu mwingine, la, ni mkewe akimwombea. Ana shida ya tumbo, hayupo hapa, bali yuko nyumbani. Bibi Phillips, amini kwa moyo wako wote. Yesu Kristo atamponya huyo ndugu kama utaamini. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote? Vema.

163 Unaamini Roho Mtakatifu yupo hapa sasa? Vema. Basi nawatakeni mfanye hivi: Ni waaminio wangapi walio hapa? Inueni mikono yenu. Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba hiyo ndiyo ishara ambayo Yesu alitoa ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi? Hiyo ndiyo aliyoupa ulimwengu, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema, hivyo ndivyo alivyoahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma."

164 Ishara ya Sodoma kwa Kanisa teule ilikuwa ni ipi? Waliona. . .Kulikuwa na uamsho mkuu uliotokea huko chini Sodoma, lakini hapa juu, katika Kanisa teule, Ibrahimu, kulikuwa na Malaika aliyejua ya kwamba Ibrahimu alikuwa ameoa, alikuwa na mke, jina lake lilikuwa Sara, Naye akauliza mahali alipokuwa.

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako." Ndipo akacheka.

Naye akasema, "Kwa nini akacheka?"

165 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu." Hiyo ni kweli? Vema basi, hilo linamfanya Yeye kuwa hapa.

166 Kama ninyi ni waaminio, kwa moyo wenu wote mkiamini, inua mkono wako, kila mmoja ambaye ni mwaminio. Sasa wewe weka mkono wako juu ya mtu fulani aliye karibu nawe, mwekee tu mkono mtu fulani aliye karibu nawe. Nitawanukulia Andiko, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hiyo ni kweli? Sasa, usijiombee mwenyewe, acha mtu huyo unayemwombea akuombee, na sasa ombeaneni, naye Mungu aliahidi, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule."

167 Na kundi lenu lote, Roho Mtakatifu yuko huko nje, Yeye yuko papo hapo juu yenu sasa. Sasa inamisheni vichwa vyenu. Basi kuna kitu kimoja tu cha kuwazuia msiupokee, hicho ni hicho kivuli kidogo cha giza. Nitamwomba Mungu amfanye ibilisi huyo aondoke hapa, ibilisi huyo wa kutokuamini, ndipo kila

mmoja wenu anaweza kuponywa. Sasa, wewe mwombee mtu uliyemwekea mikono.

168 Baba wa Mbinguni, tunawaleta wasikilizaji hawa Kwako sasa, kwa kuwa umejithibitisha kuwa hai baada ya miaka elfu moja mia tisa. Maandiko yako yanasema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ee Bwana, Wewe uko hapa, Nguvu Zako ziko hapa, watoto Wako wanaomba, Roho Wako yupo hapa. Tunaondoa shaka hili, tunamshinda Shetani kwa nguvu za Mungu.

169 Katika Jina la Yesu, ibilisi na awaachilie watu hawa, kila mmoja wao!

170 Nguvu za Mungu na zishuke katika jengo hili, jalia kila mtu hapa apate kuwekwa huru na nguvu za maradhi na nguvu za giza. Roho Mtakatifu na awe na haki ya kuingia katika kila moyo. Tujalie, Bwana. Tunawakabidhi Kwako.

171 Katika Jina la Yesu Kristo, ninazitoa nguvu chafu za Shetani! Jalia aondoke kwenye kusanyiko hili na kila mmoja wao aponywe.

172 Mnamwamini? Mnaamini mmeponywa? Sijali jinsi ulivyolemaa, jinsi ulivyo mahututi, ninakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, katika Uwepo wake Yeye anayejua yote kukuhusu, simama kwa miguu yako na upokee uponyaji wako, sijali kuna shida gani, simama. Amina.

173 Hilo hapo. Bwana asifiwe! Umeponywa, Mwenyezi Mungu anakuponya, ninalitangaza, katika Jina la Yesu Kristo, ninapoirudisha ibada hii kwa Ndugu David.

60-0331 Tangu Wakati Huo
Municipal Auditorium
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org